
MEDIA COUNCIL OF KENYA




# MIONGOZO YA KUANGAZIA UCHAGUZI

## 2022

www.mediacouncil.or.ke
mediacouncilofkenya
@mediacouncilk

@Haki Miliki 2021
Orofa ya chini,
Jengo la Britam Centre,
Mara /Ragati Road Junction, Upper hill,
S.L. Posta 43132 -00100 Nairobi, Kenya
Nambari ya Simu: +254(020)2737 58/+254(020) 271 6266,
Simu ya Rununu: +254(0) 727 735 252
Barua Pepe: info@mediacouncil.or.ke
www.mediacouncil.or.ke

## KAULI YA KUJITOLEA YA WAHUSIKA

| TAASISI | JINA | SAINI |
|---|---|---|
| Wizara ya Habari Teknolojia ya Mawasiliano na Masuala ya Vijana | Kanali (Mustaafu) Cyrus Oguna | |
| | Judy Munyinyi | |
| Baraza kuu la Vyombo vya Habari | Maina Muiruri | |
| Shirika la Habari la Standard | Orlando Lyomu | |
| Chama cha Wanahabari | Erick Oduor | |
| Baraza kuu la wahariri | Churchill Otieno | |
| TV 47 | Abubakar Abdullahi | |
| Chama Cha Waandishi wa Habari, Kenya | William Oloo Janak | |
| Wakala /Taasisi ya Habari ya Kenya -KNA | Joseph K. Kipkoech | |
| Muungano wa wanawake kwenye vyombo vya habari | Judie Kaberia | |
| Umoja wa watangazaji wa mtandao wa dijitali | Joel Karanja | |
| Mtandao wa Vyombo vya habari vinavyomilikiwa na jamii vya Kenya | Tom Mboya | |
| Umoja wa wasimamizi wa vyombo vya habari vinavyomilikiwa na jamii | Kelvin Nyangweso | |
| Wanahabari kuhusu haki za binadamu | Sammy Muraya | |
| Idhaa ya Kitaifa ya KBC | Kennedy Osir | |
| Shirika la Habari la MediaMax | Erick Obino | |

## KAULI YA KUJITOLEA YA WAHUSIKA

| TAASISI | JINA | SAINI |
|---|---|---|
| Shirika la Habari la Royal Media | Joe Ageyo | |
| Wakfu wa Chumba cha Habari cha Wanawake | Njeri Rugene | |
| Chama cha wanahabari wanaoripoti masuala ya bunge nchini | Duncan Khaemba | |
| Kituo cha Capital FM | Benard Momanyi | |
| Chama cha wanahabari wanaoripoti masuala ya siasa nchini. | Kennedy Murithi | |
| Umoja wa wanahabari huru | Winnie Kamau | |
| Chama cha wanahabari wanaoripoti masuala ya ugatuzi | Hillary Mageka | |
| Shirika la Habari la Nation | Benard Mwinzi | |
| Chuo Kikuu cha Nairobi | George Nyabuga | |
| Chuo Kikuu cha Aga Khan | Joseph Odindo | |

## JEDWALI LA YALIYOMO


Kauli ya shukrani viii
Utangulizi x
Miongozo kwa ufupi xi

**HAKI NA WAJIBU 1**
1)Kuwajibikia raia 1
2)Kuwajibikia mgombeaji 1
3)Kuwajibikia taifa 2
4)Maadili 2
5)Wajibu wa vyombo vya habari 5
6)Wajibu wa vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali 7
7)Wajibu wa vyombo vya habari vinavyomilikiwa na jamii/ vyombo vya ndimi asili 7
8)Wajibu wa wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari 8
9)Wajibu wa taasisi za serikali 8
10)Wajibu wa wadhibiti wa Vyombo Vya Habari 9
11)Usalama wa wanahabari 9
12)Kushughulikia janga la Korona (Covid-19) 10
13)Midahalo ya siasa 11

**MADHARA NA HATIA 12**
14)Matamshi ya chuki 12
15)Kuripoti kwa kuelewa hisia za mizozo katika jamii 13
16)Kuripoti kwa kuelewa masuala ya jinsia 14
17)Kuwaangazia watu wanaoishi na ulemavu 16
18)Kuwaangazia vijana 16

**HABARI/VIPINDI NA MIFUMO YAKE 18**
19)Mitandao ya jamii, vyombo vya dijitali 18
20)Habari za uongo 18
21)Kura za maoni 19
22)Matangazo ya moja kwa moja, simu za kupokewa studioni na vipindi vya mijadala 21
23)Matangazo ya kusifia wanasiasa na matangazo yaliyolipiwa 21

## JEDWALI LA YALIYOMO


**UTEKELEZAJI MIONGOZO HII** **23**

24)Miongozo ya uhariri /Sera za vituo vya habari 23

25)Malalamiko 23

26)Kufuatilia kazi ya vyombo vya habari 23

**MAREJEO/DONDOO** **25**

Kiambatisho 1 26

**RATIBA YA UCHAGUZI WA 2022** **28**

**MDUARA WA UCHAGUZI** **34**

## KAULI YA SHUKRANI

Tungependa kumshukuru mwenyekiti wa kamati ya kiufundi kuhusu shughuli ya kuhakiki Miongozo ya Uchaguzi, Bw Joe Odindo, kwa kuongoza kazi ile na kukipitia kijitabu hiki. Zaidi ya hayo tunatambua michango ya wanachama wa kamati ambao ni David Aduda, George Nyabuga, Njeri Rugene, Judie Kaberia, Jane Godia, Sophia Wanuna, Bernard Mwinzi, Shitemi Khamadi, David Mwere, David Okwemba, Alex Mwangi, Alphonce Shiundu, Felix Olick, Samuel Maina, Sarah Kimani, Jamila Mohamed, Henry Owino, Moses Njagi, Ahosi K'Obonyo na Oscar Obonyo.

Tumepata usaidizi mkubwa kutoka kwa bodi ya Baraza kuu la Vyombo vya Habari iliyoongoza ushauri wa kisera na mwelekeo kwa ujumla. Tuwashukuru vilevile watumishi wa Baraza hilo kwa kupokea dhana ya mradi huu na kuhakikisha kazi imefanywa na kijitabu hiki kimeandaliwa. Tuwataje Bw David Omwoyo (Afisa Mkuu Mtendaji wa Baraza), Bw Victor Bwire (Mkurugenzi, Mafunzo ya Vyombo vya Habari na maendeleo ya Vyombo hivyo, Bi Dinnah Ondari (Meneja - Uhuru wa wanahabari, usalama na utetezi) na Bw Julius Sigei (Afisa Mwanadamizi -viwango vya mafunzo na umbunji wa mitalaa). Juhudi zao ziliisaidia kamati pakubwa wakati wa kuandaa upya kijitabu hiki. Tunatambua kazi ya Bw Jerry Abuga, Bi Lorine Achieng' na Wilbur Alusiola kwa kuhariri mswada wa kijitabu hiki, kusanifu kijitabu na kubuni muundo wake.

Tungependa kushukuru Chama cha Wahariri cha Kenya- KEG, Chama cha kutetea Maslahi ya Wanahabari- KUJ, Chama cha Wanahabari huru cha Kenya- KCA, Chama cha wanawake wa Vyombo vya Habari-AMWIK, Chama cha Wamiliki Vyombo vya Habari –MOA, Chama cha umiliki wa kijamii wa Vyombo vya habari –KCOMNET, Chama cha wanahabari wa masuala ya Bunge, na Chama cha Wanahabari wa masuala ya Ugatuzi, kwa michango yao iliyotia nguvu kwenye ukamilishaji wa kijitabu hiki.

Tutambue pia michango ya Mashirika ya Habari yafuatayo; Shirika la Habari la Nation, Shirika la Habari la Standard, Wakala/Taasisi ya Habari ya Kenya-KNA, Shirika la Habari la MediaMax, Shirika la Habari la Radio Afrika, Shirika la Utangazaji la Taifa- KBC, Shirika la Habari la Royal Media, na Shirika la Jamii la Article 19. Tunawashukuru vilevile wote waliohusika kwenye vikao vya washikadau na ukaguzi.

Mwishowe, tungependa kuyashukuru mashirika yafuatayo ya kimataifa hasa kwa kuwa tumetumia nakala za Miongozo yao; Shirika la utangazaji la Jumuiya ya Madola, Kituo cha Afrika Kuhusu viwango tajika vya Vyombo vya habari, Kituo cha Kimataifa kuhusu wanahabari-ICJ, Shirika la Kufuatilia kazi ya Vyombo vya habari ili kukuza Uchaguzi wa kidemokrasia (Taasisi ya Taifa kuhusu Demokrasia), Shirika la Ufadhili wa Kimataifa

## KAULI YA SHUKRANI

wa Vyombo vya Habari, Shirika la UNESCO, Maripota wasio na Mipaka na Shirika la Kimataifa la miegemeo ya Kifaransa-OIF, Taasisi ya Sera za Umma-PPI, Mtandao wa Uanahabari wenye maadili, na Shirika la Jamii la Article 19 - tawi la Afrika Mashariki, Bunge la Taifa, Seneti na vyama vya Siasa chini ya mwavuli wa kamati ya vyama vya siasa, Baraza la Magavana na Tume Huru ya Mipaka na Uchaguzi kwa michango yao kwenye shughuli nzima ya kutunga miongozo hii ya uangaziaji uchaguzi.

# UTANGULIZI

**Tukiwa** wahariri, wanahabari, wafanyakazi kwenye vyombo vya habari, wamiliki na mameneja wa vyombo vya habari,

**Tukielewa** umuhimu wa uchaguzi mkuu,

**Tukishauriwa** na ari ya kutaka kuwezesha ufanyike uchaguzi huru, kwa njia ya haki na inaoaminika, kwa njia yenye uwazi na kuzingatia utaratibu wa kidemokrasia,

**Tukifahamu** kwamba katiba yetu inatoa nafasi kuwe na uhuru, mawazo huria kwa aina zote za Vyombo vya Habari huku ikitoa idhini kwa raia wote wawe na uhuru wa kujieleza, ambao pia unashirikisha uhuru wa kutafuta, kupokea na kutoa habari na mawazo,

**Tukitambua** kwamba uhuru wa vyombo vya habari unaandamana na wajibu na majukumu yake,

**Tukijitolea** kuwasaidia wapiga kura kufanya uamuzi unaotiwa msingi na ufahamu wa mazingira yao,

**Tunaamua** na kuweka nadhiri ya kutii na kuifuata miongozo hii wakati wote wa kuangazia uchaguzi



## MIONGOZO KWA UFUPI

Miongozo hii kwa ajili ya kuangazia uchaguzi imetokana na ushirikiano baina ya vyombo vya habari na mashirika mengine yanayoshughulika katika kuhakikisha kwamba uchaguzi unakuwa wa kuaminika, unaoweza kuthibitishwa, ulio huru, unaokubalika, unaofanyika kwa njia ya amani na unaotii kanuni za demokrasia na kwamba unaangaziwa ifaavyo na vyombo vya habari.

Miongozo hii inarejelea msingi wa Kanuni za utendakazi wa kazi ya uanahabari nchini Kenya, maagizo ya Katiba ya Kenya -2010, na sheria zilizopo.

Kijitabu hiki kimepangwa kwa njia laini ili kumpa msomaji yeyote wepesi wa kukisoma.

Miongozo hii inangaazia masuala kadhaa ikiwemo

a) Haki na uzingatiaji maoni ya pande zote
b) Ufisadi (namna unavyowaathiri washirika katika vyombo vya habari)
c) Kushirikisha jinsia zote
d) Ushirikishaji wa wengi na kukaribisha mitizamo tofauti tofauti
e) Uanahabari unaotahadhari maana ipo mizozo na hisia za makabiliano katika jamii
f) Kura za maoni
g) Uangaziaji wa pande zote kwa njia ya usawazishaji
h) Elimu ya jamii
i) Simu studioni/kuwashirikisha wasikilizaji
j) Uanahabari wa mitandao ya jamii
k) Usalama wa wanahabari
l) Habari za uongo
m) Kuangazia watu wanaoishi na ulemavu
n) Wamiliki vyombo vya habari na wahariri
o) Janga la Korona (Covid 19)
p) Wadhibiti/waratibu
q) Vyombo vya habari vya kijamii na vinavyotangaza kwa lugha asili za Kenya
r) Midahalo ya urais na mingineyo
s) Matangazo ya moja kwa moja
t) Shughuli za kisiasa za washirika kwenye vyombo vya habari

Miongozo hii inanuia kuwasaidia wanahabari na washirika wengine katika vyombo vya habari kutoa nafasi ya uangaziaji uchaguzi kwa njia kamilifu, sahihi, isiyopendelea upande wowote na yenye haki, ili kuwawezesha wapiga kura kufanya uamuzi unaowafaa. Miongozo hii inawalenga washirika wote kwenye sekta ya vyombo vya habari, vyombo binafsi, vya kijamii au vinavyomilikiwa na serikali – vilevile miongozo hii inawalenga washirika wengine walio nje ya vyombo vya habari lakini wanashiriki katika kusimamia uchaguzi au kuratibu namna uchaguzi unafanywa, na kwamba wameipokea na kuikubali miongozo hii.

# HAKI NA MAJUKUMU

Kwenye utaratibu mzima wa uchaguzi wowote ule, zipo haki za namna tatu

i) Haki ya mpiga kura kufanya uamuzi unaofaa kwa sababu amefahamishwa ifaavyo

ii) Haki ya mgombeaji kusambaza hoja zake ili aeleweke na umma

iii) Haki ya vyombo vya habari kuripoti matukio kwa njia huru, huku vikitoa hoja kuhusu maswala muhimu kwa umma kwa njia huru

## 1. Kuwajibikia raia

Wajibu wa vyombo vya habari msimu wa uchaguzi ni kuhakikisha kwamba mpiga kura amepata habari zifaazo kumwezesha afanye uamuzi unaomfaa ufikapo wakati wa kupiga kura. Kwa hivyo vyombo vya habari vina jukumu la kufuatilia na kuangazia shughuli za uchaguzi kwa njia inayompa mpiga kura habari sahihi, zinazoweza kutegemewa kuhusu utaratibu mzima wa uchaguzi. Baadhi ya mambo ambayo mpiga kura anafaa kuyaelewa kupitia juhudi za vyombo vya habari ni sheria za uchaguzi, utaratibu wa uchaguzi, maswala yanayoibuka kwenye misururu ya kampeni, vyama vya siasa na wagombeaji, na vilevile usalama uchaguzini. Habari hizi zitamwezesha mpiga kura kufahamu haki ya kutekeleza jukumu lake la kidemokrasia bila woga, kutishwa au bila kulazimishwa.

Vyombo vya habari pia vinafaa kumpa mpiga kura nafasi ya kusikika; iwe moja kwa moja hivi kwamba mpiga kura anapata fursa ya kujieleza na asikike, au kuwezeshwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kuhakikisha hoja zake na kauli zake zinasambazwa na vyombo vya habari- iwe kupitia namna ya uangaziaji au hata kupitia kura za maoni.

Vyombo vya habari vina jukumu la kufafanua na kufichua ukweli uliomo kwenye hadithi zinazosambazwa kuelezea asili ya suala fulani, ubaguzi dhidi ya makundi fulani, kukomesha habari za uongo, juhudi za kusambaza uongo na propaganda za kusifia watu fulani.

## 2. Kuwajibikia mgombeaji

Vyombo vya habari vinafaa kutoa habari kwa usahihi, kuzingatia haki, kuangazia pande zote, na kwa njia isiyoegemea upande wowote kila vinapoangazia uchaguzi. Vyombo hivyo vinafaa kuonyesha kwamba vinawapa nafasi wagombeaji wote na vyama vyote vya siasa, au kwamba wahusika hao pia wanahojiwa na kuulizwa maswali – vyama vya kisiasa ambavyo ni vidogo, na wagombeaji wasiojulikana wasichukuliwe kwa njia inayoshusha heshima zao. Uangaziaji wa haki unaotoa nafasi kwa pande zote kusikika vilevile unamaanisha kwamba hata taarifa za matukio ya uchaguzi, na wakati ambapo yanaripotiwa, unarejelea hoja za vyama tofauti tofauti au wagombeaji tofauti tofauti.

## 3. Kuwajibikia nchi

Vyombo vya habari kwa pamoja huchukuliwa kama raia wa nchi; kwa hivyo vina jukumu la kuhusika katika kujenga nchi iliyo salama na kujali mustakabali wake. Kutokana na hilo vyombo vya habari vinafaa kutumia nafasi muhimu viliyonayo msimu wa uchaguzi kupigania utulivu katika nchi, kuzuia mizozo na migongano, ikiwemo vurugu za kijinsia kwa kupigia debe uzingatiaji utiifu kwa sheria na utendakazi wema wa taasisi za serikali. Hilo linashirikisha kupigania kuwepo heshima na utawala unaotii katiba ya nchi kwa viwango vya kimataifa. Vyombo vya habari vilevile vinafaa kujenga mifumo ya kuzuia mizozo ya ndani katika vyumba vya habari. Mizozo hiyo inaweza kuathiri au kushawishi namna ambavyo vinaangazia uchaguzi. Vyombo vya habari vina jukumu la kuonyesha misimamo mbalimbali kwenye matangazo yake ya uchaguzi, ikiwemo misimamo ya makundi ya wale wanaopuuzwa au jamii zilizotelekezwa. Kuripoti uchaguzi kwafaa kuelewa tofauti zilizopo baina ya jinsia ili kuzipa nafasi jinsia zote, kuwapa raia nafasi sawa wakiwa vyanzo vya habari na wahusika kwenye habari.

## 4. Kanuni

Kila vinapoangazia uchaguzi, vyombo vya habari/wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo vya habari wanafaa kuzingatia kanuni za utendakazi wa kazi ya uanahabari siku zote:

***i) Usahihi na haki***

Vyombo vya habari siku zote lazima kuhakikisha kwamba taarifa zake za habari ni sahihi, za ukweli, zina haki, zinaangazia pande zote na kwamba yale yanayochapishwa yanaweza kuthibitishwa.

***ii) Kushirikisha mawazo mbadala***

Vyombo vya habari vinafaa kuandaa na kuchapisha taarifa zinazoangazia pande zote zinazorejelea kauli zote zilizotolewa kuhusu jambo Fulani. Namna ya kuchagua hoja za kuchapisha pia yafaa kuonyesha mitizamo mingi inayoibuka kwenye mjadala wa kitaifa unaoendelea. Tahariri zinazochapishwa na makala yaliyolipiwa ili kuchapishwa au kuangaziwa yote yanafaa kutambuliwa waziwazi ili yatofautishwe na habari

***iii) Usiri wa vyanzo muhimu vya habari***

Vyombo vya habari vinawawajibikia watu na taasisi ambazo vinaziangazia na vilevile wajibu kwa jamii nzima. Kwa hivyo wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo vya habari wanafaa kulinda vyanzo vya habari; kuweka siri majina ya wale waliofichua yale muhimu. Licha ya hiyo vyombo vya habari havitatumia vyanzo vya habari visivyotajwa majina

kuendeleza agenda zao binafsi na kuchapisha uongo.

***iv) Haki ya kusikika***

Vyombo vya habari vitampa mtu yeyote au shirika lolote nafasi ya kuelezea upande wake akiwa ameangaziwa kwa njia inayomdhulumu au kumfedhehesha, Wakati wowote vyombo vya habari vikipeperusha ripoti zisizo sahihi na zinazomtaja mtu vibaya, mhusika anafaa kupewa nafasi kuelezea upande wake.

***v) Uadilifu***

Wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo vya habari lazima watekeleze majukumu yao kwa njia inayotii Kanuni ya Utendakazi wa kazi ya Uanahabari nchini Kenya. Yafaa pia waonyeshe kwamba wanawaheshimu watu huku wakijaribu juu chini kujenga heshima ya watu kwenye taaluma ya Uanahabari. Ieleweke kwamba ufisadi ni tishio kuu kwa kazi ya uanahabari, kwamba unaweza kuharibu heshima zinazofaa kupewa vyombo vya habari ili kuendelea kusikizwa na kuaminika, tumekubaliana sote kwamba mshirika katika vyombo vya habari:

a) Hatakubali au kupokea rushwa
b) Hatatumia visivyo nafasi yake ya Uanahabari
c) Hatatoa nafasi za mapendeleo kwa mwanasiasa yeyote au chama chochote cha kisiasa
d) Hataandaa taarifa zinazolenga kufaa maslahi binafsi ya watu, maslahi ya chama, kabila au dini.
e) Hatawaharibia watu sifa
f) Hataendeleza na kupalilia matamshi ya chuki, kuwachochea watu kufanya vurugu na kufanya propaganda
g) Hatatangaza matokeo ya uchaguzi ambayo bado kuthibitishwa.
h) Hatachapisha habari ambazo ukweli wake haujathibitishwa.
i) Hatabadilisha tarakimu, takwimu na ukweli uliopo

***vi) Maneno machafu, lugha ya matusi na mielekeo ya kuchukiza***

Vyombo vya habari havitachapisha maneno machafu, matusi na taarifa zinazochukiza- ipo idhini ya kufanya hivyo iwapo itakuwa ndiyo njia ifaayo zaidi kuufahamisha umma ifaavyo au iwapo habari ile haitakuwa na mashiko bila matamshi kama hayo

Kuchapisha picha za miili ya watu ikiwa imekatwakatwa, visa vya watu kutokwa na damu na umwagaji damu, maeneo ya kutisha kwafaa kuepukwa – ipo idhini iwapo kuchapisha picha hizo na video kama hizo ndio kuuhudumia umma vyema.

Iwapo picha hizo au video lazima zitumike; kuchapishwa au kupeperushwa, itafaa umma uonywe kwamba zipo picha zinazotatiza au zipo habari zinazotatiza.

***vii) Faragha***

Licha ya kwamba washirika kwenye siasa, wakiwa watu ambao maswala yao huangaziwa mbele ya umma, kumaanisha wameachilia shughuli zao nyingi kuangaziwa, ni muhimu kwa vyombo vya habari kuelewa kwamba watu hao pia wana maisha binafsi yanayofaa kupewa faragha za kutosha, ikiwemo maisha ya familia na jamii zao. Kwa hivyo wakishughulikia watu wenye nafasi kama hizi, wanahabari/washirika katika vyombo vya habari watahakikisha:

a) Linganisha haja ya umma kupata habari / haki ya umma kufahamishwa na haki ya mwanasiasa / mtu yeyote maarufu kupata nafasi ya kufanya shughuli zake binafsi.

b) Jiulize ni kwa njia ngani habari unazotafuta kutoka kwa mwanasiasa huyo zinahusika kwenye majukumu yake ya umma. Na upo mwingiliano wowote baina ya mambo yake na shughuli za vyombo vya habari?

c) Lenga maswala na habari zinazohitajika kwenye shughuli za uchaguzi na utaratibu wa kidemokrasia

d) Usiingilie na kuuliza maswali kuhusu maisha binafsi ya mwanasiasa bila idhini yake, mwelekeo kama huo unakubalika tu iwapo yapo mahusiano baina ya maisha yake binafsi na mambo ya umma.

e) Usitumie habari kuhusu boma la mtu, familia yake, dini, kabila/jamii, afya yake, mahusiano yake ya kimapenzi, maisha binafsi na shughuli zake za faragha – ipo idhini tu iwapo maswala haya yana mwingiliano na shughuli zake za umma kwa hivyo umma una haki ya kuzijua.

f) Usiingilie au kuuliza maswali kuwahusu watu wenye uhusiano binafsi na mwanasiasa iwapo wao sio wahusika kwenye siasa – ipo idhini iwapo yale wameyahusika yanaathiri shughuli za umma.

***viii) Kuingilia majonzi na mishtuko ya watu***

Vurugu ambazo hutokea wakati wa uchaguzi na majonzi ya watu mara nyingi hupewa umuhimu kama habari kuu, lakini waathiriwa wengi huwa hawajui namna ya kujihusisha na vyombo vya habari. Wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo vya habari wanapaswa kujiepusha na hali ambapo wanawatumia vibaya waathiriwa hao- yafaa waheshimu faragha za waathiriwa hao. Iwapo taarifa anayoshughulikia mwanahabari inahitaji waathiririwa kuhojiwa, basi taarifa hiyo yafaa kuandikwa na kupeperushwa kwa njia inayojali maslahi ya walioathirika. Katika kushughulikia visa vyenya majonzi na

mishtuko, vyombo vya habari/wanahabari wanapaswa:

a) Kujali maslahi ya wahusika kila anapokusanya habari
b) Kujitambulisha na kupata idhini ya jamaa wa familia anayetegemewa na familia ile kabla kuingia nyumbani kwao- boma la watu si maeneo ya umma, kutafuta habari.
c) Kuwa mwangalifu katika kutumia picha na majina ya wahusika- usichapishe au kupeperusha iwapo upo uwezekano wa kuwaathiri watu wahusika kwa namna yoyote ile

***ix) Kamera na vifaa vya kunasa sauti kisiri***

Kunasa sauti za watu au kwa kamera kwa njia ya siri hupalilia mjadala kuhusu kanuni za kazi na ukiukaji sheria. Kwa hivyo, swala hilo yafaa vyombo vya habari na wanahabari waichukulie kwa namna ya;

a) Kutomnasa mtu kwa kamera au sauti yake bila mwenyewe kujua. Ipo idhini ya kunasa kwa siri kwa ajili ya kumlinda mwanahabari kukitokea mashtaka kuhusu taarifa aliyoifanya, vilevile iwapo taarifa anayofuatilia ina umuhimu mkubwa kwa umma huku mwanahabari akiwa hana njia nyingine ya kupata habari hiyo.
b) Kabla kunasa mazungumzo ya simu ili yatumike kwenye taarifa, au kwenye matangazo ya moja kwa moja, kwanza wafahamishe wahusika kwamba simu hiyo inarekodiwa na mazungumzo yatatumika kwenye taarifa za habari. Hata hivyo suala hili ni tofauti na pale ambapo mazungumzo ya simu ni yale yamefanywa kwenye stesheni zenye vipindi vya watu kupiga simu studioni kuchangia mijadala ambayo inapeperushwa moja kwa moja, na:
c) Kutowapiga picha watu wakiwa wanapiga kura ndani ya kituo cha kupiga kura kwa sababu kura ya mtu ni siri.

## 5. Wajibu wa chombo cha habari

Ili kuwe na uangaziaji uchaguzi kwa njia safi na nyororo ya kitaalamu, chombo cha habari kinafaa:

i) Kuhakikisha kwamba wanahabari wake na washirika wengine kwenye vyombo wanafanya kazi katika mazingira yanayoifaa kazi ile
ii) Kuwapa wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo uhuru wa kufanya kazi yao.
iii) Kuwalipa wanahabari mishahara inayoendana na umuhimu wa kazi yao, wape vifaa vya kufanya kazi na mafunzo kuhusu namna ya kuangazia uchaguzi
iv) Kuhakikisha usalama wa wanahabari/washirika wengine katika vyombo vya habari na usalama wa vifaa vyao vya kazi hasa kupitia mipango ya bima. Wanahabari na

washirika wengine kwenye vyombo vya habari ambao wamejeruhiwa kazini na vifaa vyao kuharibiwa yafaa walipiwe fidia

v) Kutii kanuni za utendakazi na viwango vya kazi vinavyotolewa na kanuni hizo

vi) Hakikisha kwamba sera za uanahabari za chombo cha habari na sera za utumiaji wa mitandao ya jamii zinatangaza masharti ya namna ya kuangazia uchaguzi.

vii) Hakikisha kwamba wanahabari/washirika kwenye vyombo vya habari na shirika la habari kwa ujumla wanalindwa kutokana na athari za kupitia mitandao ya jamii zinazotishia usalama wao.

viii) Toa huduma za ushauri nasaha wa kisaikolojia kwa wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari kuhusu matatizo wanayokumbana nayo wanapoangazia na kufuatilia shughuli za uchaguzi

ix) Wanahabari wa kike na washirika w akike kwenye vyombo vya habari hukabili hatari za namna tofauti na wanaume kwa sababu ya jinsia yao. Wasimamizi katika vyumba vya habari yafaa wawe wanakumbuka haya kila mara wanapowatume nje kufuatilia shughuli hatari iwe uchaguzini au nyingine.

x) Hakikisha kwamba wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari wanaoangazia uchaguzi wamepata vitambulisha mahsusi kwa jukumu hilo. Mbali na vitambulisho wakuu wa mashirika ya habari wanapaswa kuwapa mavazi maalum ya kuwatambulisha makoti ya, kofia ambazo zafaa kuvaliwa wakati wote mwanahabari yupo kazini

xi) Vyombo vya habari, kwenye masuala ya kisiasa, vinapaswa kuchukua msimamo wa kadri hivi kwamba haviegemei upande wowote. Ikitokea kwamba chombo kimechukua msimamo wa kuunga mkono mgombeaji fulani au chama fulani, chombo kama hicho kinafaa kukumbuka kwamba msimamo huo unawatia hatarini wanahabari wa chombo hicho kadri wanapofuatilia shughuli za uchaguzi.

xii) Hakikisha kwamba mwanahabari anayenuia kuwania kiti uchaguzini au anayeamua kumfanyia kazi mgombeaji fulani au chama cha siasa wakati wa uchaguzi anajiuzulu kutoka kwenye chumba cha habari miezi sita kabla siku ya uchaguzi.

xiii) Utaratibu ambapo vyombo vya habari vinafuatilia matokeo ya uchaguzi kutoka vituo vya kupigia kura na kufanya hesabu ya kura hizo huchangia katika kuboresha makali ya kubaini makossa uchaguzini. Licha ya hivyo vyombo vya habari havitawatangaza washindi kwenye nyadhifa zozote zile, kabla taasisi maalum inayoongoza uchaguzi imetoa tangazo rasmi.

## 6. Wajibu wa vyombo vya habari chini ya umiliki wa serikali

Wakala/Taasisi ya Habari ya Kenya (KNA), Shirika la Utangazaji la Taifa (KBC), na taasisi ya MyGov kwa pamoja yana wajibu katika msimu wa uchaguzi kuufahamisha umma yanayotokea kwenye utaratibu mzima wa uchaguzi, huku yakiangazia maswala muhimu na kuwaelimisha wapiga kura.

Likiwa shirika la Utangazaji la Taifa, KBC lina wajibu wa kuangazia uchaguzi kwa njia ya haki na usawa kwa wahusika wote huku likitoa nafasi kwa hoja zinazotofautiana kupeperushwa. Mbali na hayo sheria inataka kwamba KBC ishauriane na Tume ya Uchaguzi na Mipaka nchini IEBC, wakati wa kampeni kabla siku ya uchaguzi wa urais au ubunge, uchaguzi katika serikali za kaunti iwe inatoa nafasi kwa vyama vya siasa ambavyo vimesajiliwa kushiriki uchaguzini kuelezea na kufafanua sera zao.

Likiwa Shirika linalofadhiliwa na umma, ili kuhudumia umma, KBC ina wajibu wa kuwaelimisha wapiga kura na kuhakikisha wanaendelea kupashwa habari muhimu msimu mzima wa uchaguzi. Vipindi vyake vinavyohusu maswala ya uchaguzi vinafaa kuifikia idadi kubwa ya watu waliosajiliwa kupiga kura. Shirika la Utangazi la KBC linafaa kufanya juhudi za kuyafikia makundi ambayo kwa desturi hutengwa kwenye utaratibu mzima wa uchaguzi, na hasa jamii za watu wachache nchini, dini ambazo hupuuzwa na wanawake.

Vipindi hivyo vinapaswa kuandaaliwa kwa njia inayozingatia haki matangazo yake yawe yasiyopendelea upande mmoja na vinafaa kuwafahamisha ifaavyo wasikilizaji kuhusiana na utaratibu wa uchaguzi, ikiwemo namna ya kupiga kura, kura hupigiwa wapi naa lini, kujisajili kuwa mpiga kura na namna ya kuthibitisha kwamba umesajiliwa, umuhimu wa kura kuwa swala la siri (hali inamwokoa mpiga kura dhidi ya kudhulumiwa), na umuhimu wa kupiga kura.

## 7. Wajibu wa vyombo vya habari vinavyomilikiwa na jamii na vyombo vinavyopeperusha matangazo kwa ndimi asili za Kenya

Ili kuhakikisha kwamba jamii, wamiliki na wafanyakazi wa vyombo hivyo hawavitumii vibaya, wasimamizi wa vyombo hivyo wanafaa:

a) Kutoaoa matangazo/habari zinazoshirikisha hoja na kauli zote kwa njia ya haki – toa nafasi kwa vyama na wagombeaji wote wanaohusika uchaguzini.

b) Kukomesha mwenendo wa kutumia chombo cha habari kuchafua sifa za wagombeaji wa viti vya siasa usiowaunga mkono.

c) Kutii kanuni ya utendakazi wa kazi ya Uanahabari nchini Kenya na Kanuni ya utungaji Vipindi kwenye Huduma za utangazaji nchini Kenya

d) Kuhaakikisha kwamba chombo hicho hakitumiki kusambaza matamshi ya chuki na uchochezi baina ya jamii au wagombeaji.

## 8. Wajibu wa wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari

Ili kuangazia uchaguzi kwa ufanisi, wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari wanapaswa:

a) Kufahamu sheria za uchaguzi na masharti yaliyopo ikiwemo taratibu za upigaji kura
b) Wafanye utafiti ufaao kuwahusu wahusika kwenye siasa na shughuli za kisiasa, ikiwemo mifumo ya vyama husika vya siasa na oparesheni zao; maswala ya fedha; umaarufu wa kimaeneo; kuuuliza maswali yanayowafaa wapiga kura, tangaza maswala ambayo raia wanataka vyama vya siasa na wagombeaji wayashughulikie.
c) Kuhakiki manifesto za vyama vya siasa na za wagombeaji ili kubaini namna wanavyotii wito wa kumhudumia raia, na kushughulikia maswala muhimu kwa rais na majukumu yao ya kikatiba
d) Kuhakikisha kwamba vitambulisho vya kazi ambavyo hutolewa na Baraza la Vyombo vya Habari la Kenya, vitambulisho vya taasisi nyingine ya usimamizi na uratibu , vipo katika nafasi sawa na vinakubalika
e) Kutii sheria zote na masharti yanayohusiana na Kanuni za Utendakazi wa kazi ya Uanahabari na wairika wengine wa vyombo vya habari msimu mzima wa uchaguzi
f) Kila wanapofuatilia shughuli za uchaguzi au waonekana kwenye televisheni wanahabarina washirika wengine kwenye vyombo vya habari wanafaa kujiepusha na mavazi yanayofanana na yale ya chama chochote cha siasa.

## 9. Wajibu wa taasisi za serikali

Vyombo vya habari vina haki ya kuendesha shughuli zao za kikazi bila woga au kutishwa. Vyombo vya habari kwa hivyo vinatarajia taasisi za serikali :

a) Kuhakikisha kwamba washirika kwenye vyombo vya habari wanaendesha shughuli zao kwenye mazingira yasiyokuwa na vurugu na vitisho sawa na inavyotajwa kwenye kifungu cha 34 cha Katiba ya Kenya 2010.
b) Kunzisha uchunguzi wa haraka na kuwashtaki wanaopanga mavamizi dhidi ya wanahabari na vifaa vyao vya kazi
c) Kuchukua hatua za kuzuia kutokea kwa udanganyifu uchaguzini, wizi wa kura na njama zinazoharibu matokeo ya uchaguzi
d) Kuandaa hesabu ya kura na ujumuishaji ufanyike kwa njia yenye uwazi kuzingatia haki huku matokeo yakitolewa punde baada ya hesabu kumalizika
e) Kuenga mahusiano safi na yenye heshima za kikazi baina ya taasisi za serikali na vyombo vya habari
f) Kuoa nafasi kwa habari muhimu zilizomo kwenye taasisi za serikali kufikiwa na vyombo

vya habari kwa ajili ya kuufahamisha umma sawa na inavyonakiliwa kwenye katiba ya Kenya (2010) na Sheria ya utoaji Habari (2016)

g) Kila mara serikali inapofanya vikao vya vyombo vya habari ni muhimu kuzingatia masharti ya kuzuia ueneaji wa janga la Korona –Covid 19.

## 10. Wajibu wa taasisi za kuratibu utendakazi wa Vyombo vya habari

Ni wazi kwamba utendakazi wa waratibu wawili wakuu wa Vyombo vya habari, Baraza la Vyombo vya habari la Kenya na Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya huongozwa na sheria zilizopo, msimu wa uchaguzi huja na mambo mengine kwa hivyo taasisi hizo mbili zafaa :

a) Kwa moyo wote, kuhakikisha utekelezaji wa kanuni za utendakazi wa kazi ya uanahabari nchini Kenya na utiifu kwa Kanuni za Upangaji vipindi miongoni mwa vyombo vya utangazaji nchini Kenya. Taasisi hizi za kuratibu vilevile zafaa kuhakikisha kwamba wanahabari na vyombo vyote vya habari vinapewa nafasi ya uhuru wa kufuatilia na kuangazia hatua zote za uchaguzi kwenye msimu huo mzima

b) Siku zote kutetea uhuru wa vyombo vya habari

c) Wekeza katika mipango ya kutoa mafunzo na elimu muhimu kwa wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo vya habari ili kuhakikisha kwamba wana ufahamu na mbinu za kuangazia uchaguzi kwa ufanisi

## 11. Usalama

Wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari wana haki ya kufanya kazi yao bila woga, bila kutishwa, kudhulumiwa, au kushambuliwa. Licha ya hiyo ifahamike kwamba hakuna tukio lolote la kumpa mwanahabari taarifa ambalo ni muhimu kuliko uhai wake. Kwa hivyo wanahabari wanapaswa daima kuchukua hatua za kuhakikisha wako salama. Wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo vya habari wafaa:

a) Kuzingatia Maadili ya kazi wakati wote wanapofuatilia na kuangazia uchaguzi

b) Kungalia kwa makini hatari iliyopo kwenye sehemu za uchaguzi zenye mizozo na jazba kabla kuelekea huko kufuatilia matukio - ikiwezekana, julisha shirika la habari wanalofanyia kazi kuhusu hali ilivyo au hata mamlaka ya serikali.

c) Wawe na haki ya kuamua aina ya matukio ambayo wanaweza kuyafuatilia iwapo wanahofia usalama wao.

d) Endeleza shughuli zao za kazi kwa uangalifu huku wakitilia maanani usalama wao na usalama wa washirika wao mfano wageni wanaowahoji na vyanzo vya habari wanaoshirikiana nao.

e) Hakikisha kuchukua msimamo wa kadri usioegemea upande wowote – hali hii itmpa mwanahabari nafasi ya kutekeleza majukumu yake kwa usalama bila hofu ya kuathiriwa.

f) Daima beba stakabadhi muhimu za kujitambulisha; kitambulisho cha taifa, kadi za Baraza la Vyombo vya habari, kadi za kuangazia uchaguzi kutoka Tume husika.

g) Beba kisanduku cha huduma ya kwanza na ni muhimu mwanahabari kujua kukitumia kisanduku hicho.

h) Vaa mavazi maalum yaliyo na nakala zinazokutambulisha kama mwanahabari zikionekana vyema – mavazi hayo yawe ya kuokoa dhidi ya hatari mfano kurushiwa jiwe n.k.

i) Ikiwezekana daima usiangazie uchaguzi huku ukisafiri ukiwa peke yako, au ukiandamana na misafara ya wagombeaji na viongozi wa kisiasa.

j) Dumisha mawasiliano na shirika lako la habari/mwajiri wako, wenzako kazini au mashirika ya huduma za usalama – halafu uwe na mpango safi wa kuondoka pale wakati wowote.

k) Angalia na kutathmini mahala ulipo ili kujua utajificha wapi kukitokea dharura au vurugu wakati unafuatilia mikutano na hadhara za kisiasa.

l) Daima beba stakabadhi zako za bima ya matibabu ili kukitokea dharura na umejeruhiwa itakuwa rahisi kupokea matibabu ya dharura.

m) Tii masharti yote yanayohusiana na janga la Korona- Covid 19, ikiwemo kuvaa mavazi ya kuzuia maambukizi, kutumia sanitaiza na kutokaribiana na watu.

Kuhakikisha usalama kutokana na athari za mitandao na nyendo za dijitali

Usalama dhidi ya athari za mitandao na nyendo za dijitali umeanza kuwa muhimu katika shughuli nzima ya kukusanya habari, kuziandaa habari zile kwa ajili ya magazeti televisheni na rediyo kupeperushwa. Kutokana na athari hizo msimu wa uchaguzi wanahabari wanafaa:

a) Wanahabari yafaa kuzipa kompyuta zao kingavirusi za tarakilishi imara ya mitandao ya kibinafsi ya dijitali(VPN) iliyohakikishiwa usalama wake ili kulinda kazi za uanahabari wanazoshughulikia ili kuhakikisha mawasiliano yao iwapo kumetokea swala la kupunguza huduma za mitandao au hata kuzima huduma hzo wakati wa uchaguzi

b) Kupata mafunzo kuhusu namna ya kukabili changamoto kadhaa za mtandao ikiwemo troli za mtandao, kuonewa na kuvurugwa, udukuaji na mashambulizi mengine ya mtandao ili kuchukua hatua muhimu za kujilinda na kulinda habari zozote ambazo mwanahabari amezihifadhi.

## 12. Kushughulikia janga la Korona –COVID 19

Kwa kuwa kufuatilia na kuangazia uchaguzi kunaandamana na kukutana na kutangamana na mikutano na hadhara za watu na wanasiasa, wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo vya habari wanapaswa kuchukua hatua za kujilinda kutokana na kuambukizwa

virusi vya Korona. Kwa hivyo yafaa;

a) Wajitenge na kutokaribiana na yeyote aliye na dalili za mafua ya namna yoyote mfano kukohoa na kuchefua
b) Wahoji watu katika maeneo yaliyo wazi wala sio kwenye vyumba. Hakikisha kwamba zipo hatua kadhaa baina yao na wageni wanaowahohi ili wasikaribiane, ikiwezekana tumia mikrofoni/kinasa sauti cha mkono mrefu.
c) Tafuta huduma za matibabu kwa haraka punde wakiona dalili mfano mwili kusikia baridi, kupungukiwa hewa ukipumua. Ni muhimu kujitenga na watu ili usiwaambukize- ndio ushauri unaofaa kuzingatiwa
d) Tumia sanitaiz a au unawe mikono mara kwa mara kwa sabuni ukitumia maji yanayotiririka. Tumia sanitaiza kwenye vifaa vya kazi zikiwemo mikrofoni/vinasa sauti
e) Tumia mavazi ya kuzuia athari za namna nyingi kila mara ukifuatilia na kuangazia mikutano ya kisiasa
f) Ukiwa umekwenda kufuatilia tukio kuliangazia iwe hospitalini, kwenye markiti au mikutano ya siasa usiweke vifaa vya kazi chini sakafuni.

## 13. Midahalo ya kisiasa

Midahalo ya msimu wa uchaguzi baina ya wagombeaji wa urais, naibu rais na ugavana imekuwa muhimu hasa kwa kuwa hutoa nafasi ya kuwapiga msasa na kuwahakiki viongozi. Midahalo ndio jukwaa la raia kuwahakiki na kuangalia kwa makini utendaji wa viongozi. Kwa hivyo vyombo vya habari vyafaa;

a) Toa nafasi kwa waombeaji wote kushiriki kwenye mdahalo wa urais bila kujali mitizamo yao ya kisiasa na vyama vyao, tabaka lao na sifa waliyonayo mbele ya umma
b) Midahalo hiyo iongozwe na wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari wenye sifa za uadilifu na wanaozingatia maadili ya kikazi. Waendeshaji midahalo wanafaa kuchaguliwa kutumia kanuni zinazokubalika katika tasnia ya uanahabari
c) Mdahalo hiyo isitumiwe kwa manufaa ya kifedha
d) Pekua kauli za wagombeaji kila wanapotoa hoja kwenye midahalo hiyo ili kuhakikisha kwamba hawatumii nafasi ile kuendeleza porojo na uongo- hakikisha kwamba wanawajibikie hoja na taarifa wanazotoa.
e) Peperusha matangazo ya midahalo na kuyachapisha kwenye vyombo mbalimbali ili kuendeleza haki na usawazishaji vilevile hakikisha imewafikia wasikilizaji na watazamaji wa tabaka mbali mbali.

## MADHARA NA HATIA

### 14. Matamshi ya chuki

Vifungu vya 33 na 35 vya katiba ya Kenya 2010 vinaidhinisha uhuru wa kujieleza na uhuru wa kupata habari, lakini pia vinanakili kwamba uhuru huo haushirikishi;

a) Propaganda inayochochea vita
b) Kuchochea vurugu katika jamii
c) Matamshi ya chuki
d) Kupalilia chuki miongoni mwa watu hasa chuki za kikabila, kuharibu sifa za watu na kuwaathiri vibaya

***Maana ya Matamshi ya chuki***

Matamshi ya chuki ni hatia chini ya sheria za Kenya. Mtu atakuwa na hatia ya kueneza chuki kupitia matamshi yake iwapo ametamka, ameandaa na kuchapisha na kusambaza habari zenye vitisho, matusi, kama vile picha za namna ile au tabia zenye nia ya kuibua chuki za kikabila. Uhalifu unaotokana na chuki nchini Kenya huchochewa na yafuatayo

a) Kutumia ubaguzi hasi unaowachukulia watu wengine kuwa wasiofaa, hasa ubaguzi unaoegemea mila na desturi za watu, jinsia, jamii na kabila na rangi ya ngozi
b) Habari zenye mielekeo ya mihemko kwenye vyombo vya habari zinazopalilia vurugu
c) Hotuba zilizojaa hisia na kauli za chuki, hasa kwenye mikutano ya siasa
d) Matangazo ya kujenga sifa za wanasiasa

***Sifa kuu za matamshi ya chuki***

a) Jumbe za kuwatisha watu, za matusi hapa na pale kutumia lugha ya mafumbo kwa lengo la kuwapotosha watu au kuwachochea.
b) Jumbe zinazolenga kundi fulani kuhamasisha chuki dhidi yao, hasa kuzingatia rangi yao ya ngozi, uraia wao, kabila na dini

***Maswali ya kuuliza kuhusiana na matamshi ya chuki***

i) Anayetoa matamshi hayo ana lengo gani, na je yafaa umma usikie matamshi yake au yanafaa kupuuzwa?
ii) Je taarifa aliyotoa ina thamani gani kwa jamii?
iii) Matamshi yake yamewafikia nani na je zipo ishara kwamba lipo lengo la kupalilia chuki?
iv) Je matamshi hayo yalitolewa maksudi kuwaathiri watu?

v) Je matamshi hayo ni hatari kwa jamii, na je yanaweza kuchochea vurugu au kusababisha madhara?

vi) Je ipo historia ya mizozo au ubaguzi hasa mahala ambapo matamshi yalitolewa?

vii) Habari zote zinazovifikia vyombo vya habari na zina sifa hizi ambazo tumeorodhesha zinafaa kufanyiwa uhakiki na upekuaji ufaao. Wanahabari na washirika wa vyombo vya habari vilevile wanapwa kutathmini Habari na kubaini ukweli wake kwa kuzingatia mahitaji ya umma ya kufahamishwa na haki za umma kupokea habari kabla ya kuchapisha habari hizo.

Kwa mujibu wa sheria za kimataifa na kifungu cha 13 cha Sheria ya Uwiano na Utangamano wa Taifa (2008), vyombo vya habari/mwanahabari:

i) Hatachapisha hotuba au matamshia ambayo moja kwa moja yanachochea vurugu au maangamizi ya jamii

ii) Hatachapisha hotuba au matamshi yenye mwelekeo wa kuchochea ubaguzi, chuki na vurugu za kikabila au kidini

iii) Akishughulikia namna nyingine za matamshi ya chuki, mwanahabari au vyombo vya habari vitumie matamshi vikiwa na nia ya kufichua yaliyosemwa, kukosoa na kukataa matamshi hayo na kiini chake. Vinginevyo, mwanahabari/mshirika katika vyombo vya Habari anapaswa:

   a) Kutowanukuu wale wanaotoa matamshi yanayochukiza hasa yanayoashiria jamii na makabila ya watu, rangi ya ngozi, tabaka na jinsia

   b) KaJiepushe na maneno hasi yanayokejeli jamii na makabila au rangi ya ngozi ya watu

## 15. Kuripoti kwa njia inayoelewa uwepo wa hisia za mizozo na migongano katika jamii

Kwa kuwa vyomboa vya habari vina wajibu muhimu katika jamii, kanuni za uanahabari unaoelewa kwamba jamii ina uwezekano wa kukumbwa na mizozo zinafaa kuwaongoza wanahabari na washirika katika vyombo vya habari wakifuatilia na kuangazi uchaguzi. Katika mazingira ya vurugu na mizozo, wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari wanafaa;

a) Wafahamishwe kuhusu asili ya mizozo hiyo inayoibuka misimu ya uchaguzi

b) Kutoa habari za uchaguzi kwa usahihi na kwa njia ya ubunifu

c) Tumia maneno kwa uangalifu ili kupunguza mizozo na kuiepusha baina ya jamii zinazozozana

d) Kutopuuza ya wale walioathirika kwa mizozo ya uchaguzi

e) Jiepushe na hali ya kuyachukulia maoni kuwa ukweli wa tukio
f) Wasaidie watu kuelewa matukio kwa kuwapa msingi wa tukio hilo na muktadha wake kupitia tathmini zisizoegemea upande wowote- jumuisha hoja nyingi na maoni ya pande nyingi.
g) Jiepushe na kuangazia mizozo ukitumia mitizamo na hoja za viongozi pekee na watu maarufu katika jamii. Kuripoti mizozo kwafaa kuchukua kauli nyingi wala sio za tabaka la walionavyo pekee. Jumuisha hoja za watu wadogo ambao watatoa misimamo inayoshikiliwa na wengi katika jamii
h) Wawezeshe raia kufahamu na kuhisisalama kwa kuripotijuhudi za kusuluhisha mizozo, kuipunguzana kudumisha amani
i) Changia katika njia za kutafuta suluhu ya mizozo
j) Jiepushe na hali ya kuwatia watu katika mazingira yanayohatarisha maisha yao
k) Elewa hisia za watu na woga walionao kuhusu jambo ili usisababishe machungu na mateso.
l) Onyesha heshima za kibinadamu hivi kwamba ukitangaza dhuluma usipuuze baadhi na kuonyesha mambo ya juu juu - mizozo yenye vurugu ina athari nyingi tena nzito.
m) Hakikisha kwamba umeelezea ni kwanini uchapishe picha fulani zinazotisha baadhi ya wasomaji/watazamaji.

Manahodha wa vipingi vya mijadala wana jukumu la kuongoza mazungumzo yanayotii sheria ili kuepuka migongano. Yafaa wawe makini kwenye matamshi wanayotoa wakati wa kuongoza mijadala. Mfano kutumia maneno kama 'watu wetu' au 'jamii yetu' kunaweza kueleweka vibaya na wasikilisaji/watazamaji, kinyume na lengo la aliyeyatumia maneno hayo. Nahodha wa kipindi anafaa kushikilia usukani kwa njia imara ili kukomesha kauli za uchochezi kutolewa na wahusika kwenye mjadala iwe studioni au kupitia njia ya simu.

## 16. Kuripoti kwa njia inayoelewa tofauti za kijinsia katika jamii

Lengo la kuripoti kwa kuelewa tofauti za kijinsia katika jamii ni kuyashirikisha maslahi ya watu wote katika jamii licha ya jinsia yao kwenye utaratibu mzima wa uchaguzi. Kuwashirikisha kwa kuangazia vizuizi vinavyowafanya wasishiriki kwa ukamilifu kwenye uchaguzi nawanaume wanafaa kupewa nafasi sawa kwenye taarifa za habari wakiwa viini vya habari au wageni kwenye vipindi. Kuripoti kwa kuelewa tofauti za kijinsia katika jamii kunahusu:

i) Kuripoti kwa kuelewa majukumu ya kila jinsia, mapungufu yaliyopo, ubaguzi kwa ajili ya jinsia ya mtu
ii) Kuhimiza usawa na haki kwa kuangazia watu wote

iii)Kuhakikisha haki na usawa kwa jinsia zote katika uchaguzi

iv)Kufichua vurugu zinazoandaliwa kuilenga jinsia fulani

Kuangazia uchaguzi unaozingatiatofauti za kijinsia katika jamii kunavitaka vyombo vya habari na wanahabari;

a) Kuangazia jinsia zote kwa njia ya haki na usawazishaji kwa kuwachagua viini vya habari na kuchapisha taarifa ili kutimiza usawa wa jinsia kwenye habari zinazopeperushwa. Vyombo vya habari na wanahabari yafaa wahakikishe;

   i) Usawa na uwakilishi wa jamii jinsia kama inavyoonekana, kusikika na kusomwa, kwenye taarifa za habari na vipindi vingine vya matukio

   ii) Uwakilishi unaosawazisha jinsia zote kama vyanzo vya habari, utoaji maoni na kutumiwa kama wataalam kwenye taarifa za habari na vipindi cha matukio. Juhudi zinafaa kufanywa ili kuwashirikisha wanawake miongoni mwa watalaamu wanaoalikwa kuchambua matukio kwenye vyombo vya habari

b) Ondoa ubaguzi  wa kijinsia kupitia kwa:

i) epuka taarifa zenye ubaguzi wa kijinsia, na zenye fafanuzi zinazowachukulia iwe wanawake au wanaume kwa njia inayoshusha hadhi yao wakati wa kuangalia sifa na majukumu ya kila jinsia katika jamii.

ii) epuka kutumia lugha inayokejeli jinsia iwe ya kike au kiume

c) Hakiki/uliza maswali kuhusu mambo yanayoathiri usawa wa kijinsia kupitia :

i) Kuchunguza kwa undani yale yanayopuuzwa kwenye suala la majukumu ya kila jinsia misimu ya uchaguzi.

ii) Kuchunguza kubaini iwapo mifumo ya uchaguzi na nchini, uchaguzi wa urais, ubunge/useneta, na kura za nyadhifa za kaunti inawazuia wanawake kushinda na wakapata nyadhifa za kisiasa.

iii) Kuchunguza mambo yanayofanya iwe vigumu kwa wanawake kuwa wagombeaji au kushinda na kupata nyadhifa za kisiasa.

iv) kutochochea vurugu dhidi ya wanawake au kupuuza maovu ambayo wanawake wanatendewa

v) Kuhunguza namna ambavyo vyama vya siasa vimetoa nafasi kwa wanawake ikilinganishwa na wanaume kugombea viti.

vi) Kuhunguza na kubaini wapiga kura wangapi wakike wamesajiliwa na vilevile wakiume ili kuona iwapo utofauti katika baadhi ya maeneo hasa yale yanayoathirika kwa mizozo

au maeneo ambayo wanawake wametengwa kwa muda mrefu.

vii) Changanua namna ambavyo jinsia zimejinyakulia nyadhifa kote ili kupata idadi ya wanawake kwa wanaume

viii) Chunguza matatizo yanayotokana na shughuli za uchaguzi hasa yale yanayochochewa na ubaguzi wa kijinsia

## 17. Kuangazia watu wanaoishi na ulemavu (PWDS)

Watu waishio na ulemavu wanafaa kuhusika kwa njia zote katika shughuli nzima ya uchaguzi. Mara nyingi walemavu hutengwa misimu mizima ya uchaguzi. Ili kundi hili liafikie haki zaokamilifu likiwa raia wan chi, vyombo vya habari vinapaswa kutoa nafasi ya mbele kisiasa ili wasikike ikiwemo kuangazia maswala yanayowahusu vinapoangazia uchaguzi. Vyombo vya habari/wanahabari wanapaswa:

a) Kuyajumuisha maswala yanayowaathiri walemavu miongoni ma maswala makuu wakati wa uchaguzi

b) Angazia walemavu kwa njia inayoinua hadhi yao na kutetea haki zao za kimsingi wakiwa raia

c) Tumia lugha inayoegemea upiganiaji haki wakati wa kuwaangazia walemavu, jiepushe na ubaguzi hasi unaowadunisha

d) Fichua sera na taratibu zinazowanyima walemavu haki zao katika shughuli za uchaguzi

e) Toa nafasi ya mbele kwa juhudi za kuwajumuisha walemavu kwenye shughuli za uchaguzi kwa namna inayotii usawa wakilinganishwa na raia wengine

f) Chunguza kiwango ambacho wagombeaji na manifesto za vyama zinaangazia maswala yanayowataathiri walemavu

g) Toa kwa usahihi na kwa haki maelezo ya walemavu kuhusu changamoto wanazopitia msimu wa uchaguzi.

## 18. Kuangazia maswala ya vijana

Nchini Kenya vijana ndio kundi kubwa sana miongoni mwa wakenya waliosajiliwa kupiga kura. Licha ya hiyo vijana hawaangaziwi ifaavyo misimu ya uchaguzi. Kutokana na umuhimu wa vijana kwenye utaratibu mzima wa demokrasia ya nchi na uchaguzi kwa ujumla, vyombo vya habari vinapaswa kutoa nafasi muhimu kwa vijana vinapoangazia uchaguzi. Kwa hivyo vyombo vya habari vinafaa :

i) Kuyajumuisha maswala yanayowaathiri vijana miongoni ma maswala makuu ya msimu wa uchaguzi

ii) Kutumia lugha inayoelewa changamoto zinazowakumba vijana. Msingi wa taarifa

kwenye vyombo vya habari wafaa kuepuka miegemeo ya ubaguzi hasi unaowachukulia vijana kuwa kundi sumbufu lisilojua amani.

iii) Kutoa kwa usahihi na kwa haki maelezo ya vijana kuhusu changamoto wanazopitia msimu wa uchaguzi.

## HABARI/VIPINDI NA MIFUMO YAKE

### 19. Mitandao ya jamii, vyombo vya dijitali

Kanuni za kimsingi za unahabari ambazo zinaongoza utendakazi kwenye vyombo asili vya habari vilevile ndizo zitatumika kuongoza shughuli za wanahabari na washirika kwenye vyombo vya dijitali na mitandao ya jamii msimu wa uchaguzi.

Hapa chini tunatoa baadhi ya miongozo kuhusu suala hili:

i) Uadilifu: Usikiuke kanuni ya kuhakikisha kazi ya uanahabari inafanywa kwa misingi ya uadilifu

ii) Viini vya habari: Mwanahabari daima anapaswa kuthibitisha habari anazopewa au kuzitoa kwenye vyanzo vya habari

iii) Usahihi: Taarifa zinazochapishwa lazima ziwe sahihi

iv) Shughuli binafsi za mwanahabari: Licha ya kwamba wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari wana uhuru wa kuandika hoja zao binafsi kwenye mitandao, mtu yeyote anayesoma hoja hizo upo uwezekano akazichukulia kuwakilisha misimamo ya shirika la habari wanalolifanyia kazi. Kwa hivyo wanahabari yafaa wafikirie kwa makini kabla kuandika hoja na kuzituma mitandaoni.

v) Misimamo ya kisiasa: Wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo vya habari wanapaswa kujiepusha na kutangaza wazi pande za kisiasa wanaozounga mkono kwa sababu hatua hiyo itaathiri uwezo wao wa kuangazia pande zote wakati wakifuatilia uchaguzi

vi) Habari za punde: Hakikisha unaelewa sera za chombo cha habari kuhusu utoaji wa habari za punde kabla kuzifyatua kwenye mitandao mbele ya matawi mengine ya shirika hilo la habari

### 20. 'Habari za uongo'

Habari za uongo ni habari zinazopeperushwa na kuchapishwa zikionekana kuwa za kweli lakini kumbe hakuna tukio lolote la kuthibitisha kwamba jambo limetokea huku viini vinavyonukuliwa pia vikiwa havijui pametokea jambo. Mara nyingi habari hizo huchapishwa kwa lengo la kuwadanganya watu. Taarifa hizo mara nyingi huchipuka kwenye mitandao. Misimu ya uchaguzi, wahusika kwenye siasa wamekuwa wakitumia mitandao kusambaza habari za uongo na zile ambazo hazijathibitishwa. Ni muhimu kutofautisha kati ya habari za uongo, ambazo zimebuniwa tu, na habari ambazo baadhi ya watu huzitaja kuwa za udanganyifu, ambazo huenda zikatokana na ukosefu wa umakini miongoni mwa wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari wakati wa kuandaa habari hizo. Zipo namna

nyingine za propaganda ambazo husambazwa ili kushawishi umma ambazo vyombo vya habari vinapaswa kuwa waangalifu visitumiwe kuzisambaza. Ili kukomesha athari za habari kama hizi, vyombo vya habari/wanahabari wanapaswa:

a) Kufichua habari za uongo na kuutangazia umma kwamba habari fulani zinazosambazwa si za kweli- ikiwezekana vyombo vya habari vinapaswa kuwafichua waliotunga habari hizo.
b) Jenga sera zinazoongoza mitandao ya jamii na kuhakikisha kwamba zimetekelezwa ili kukuza kanuni za utendakazi wa uanahabari katika nyanja za mitandao.
c) Wasitumie au kuchapisha habari ambazo haziwezi kuthibitishwa.
d) Kutumia teknolojia ya kisasa ya mitandao kutafuta habari za uongo na kuzifichua.
e) Kuumia njia zinazoaminika kuthibitisha habari na hata picha na nakala za video ambazo huenda ni za uongo
f) Daima thibitisha habari zote zinazochapishwa kwenye mitandao ya jamii kabla hata kuzisoma zote
g) Tumia mbinu za kubainisha ukweli wa habari kuzithibitisha kabla kuzichapisha au waweza kuwatafuta wataalamu wa kuhakiki habari kupata ukweli wake

## 21. Kura za maoni

Kura za maoni katika msimu wa uchaguzi zinatumika kupima mielekeo ya mawazo ya watu na mitizamo yao. Hata hivyo, ili kuhakikisha usahihi wa ripoti za utafiti, yafaa kwanza shughuli ile ifanywe kuambatana na njia zilizopo za kisayansi. Kutokana na hiyo vyombo vya habari/wanahabari wanapaswa:

i) Kabla kutangaza matokeo ya mashirika ya kutafiti kura ya maoni yaliyofanywa na mashirika hayo yenyewe watafuata sheria ya Uchaguzi na Kura za maoni inayoelezea namna utafiti huo unafaa kufanywa na kuangaziwa na vyombo vya habari
ii) Wapate habari kuhusu njia zilizotumika kuendesha utafiti huo, wapate matokeo rasmi ya utafiti huo halafu tafuta maoni na hoja za wataalamu kuhusu ubora wa njia zilizotumika kufanya utafiti huo vilevile ufafanuzi wa matokeo hayo.
iii) Maelezo ya watu waliohojiwa kwenye utaratibu wa utafiti (sauti zao zilizonaswa) kwa namna ya kupita tu bila mpangilio maalum, sio utafiti wa kisayansi jinsi inavyotakikana. Haya yote yanafaa kupewa wanahabari ili kuonyesha upana na undani wa shughuli ya maoni kuhusu swala linalojadiliwa nchini

Kufuatia mapendekezo ya Shirikal a utafiti wa kura za maoni duniani (WAPOR) na Sheria ya kuchapisha kura za maoni (Nambari 39 ya Mwaka 2012) vyombo vya habari/wanahabari

wanapaswa kushauriwa kwa maswali yafuatayo ili kubaini usahihi wa utafiti wa kura za maoni na kuzitumia kwenye taarifa zao

1) Nani alifadhili utafiti?
2) Nani alilipia gharama za utafiti?
3) Mbona utafiti ulifanywa?
4) Nani aliendesha utafiti huo?
5) Ni maeneo gani ya kijiografia yaliangaziwa wakati wa kukusanya maoni?
6) Ni watu wangapi walihojiwa?
7) Kundi la watu waliohojiwa walikuwa wa matabaka yapi na je kiswango chao kiliwakilisha matabaka yote?
8) Njia zipi zilitumika kupata makundi ya kuulizwa maswali?
9) Majibu yalikuwa yapi na idadi ya wale waliokataa kujibu maswali?
10) Ni maswali aina gani yaliulizwa?
11) Aina gani ya wafanyakazi katika shirika la utafiti walihusika katika kukusanya habari muhimu kwenye utafiti huo?
12) Utafiti ulichukua muda gani?
13) Je viwango vya uwezekano wa kukosea vilikuwa vya nyuzi gani?
14) Majibu yalikuwa yapi?

Kura za maoni za papo hapo kwenye Rediyo, Televisheni na mitandao ya jamii

a) Matokeo ya kura za maoni ambazo hufanywa kupitia vipindi vya rediyo televisheni na mitandao kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu hufanywa kwa njia isiyozingatiasayansi ya kura ya maoni kwa hivyo inafaa umma kuonywa kwa shughuli hiyo haiwakilishi maoni haswa ya watu.
b) Idadi ya watu wanaoshiriki kwenye shughulli hii, wanashiriki kutoka upande gani, yafaa kuelezwa wasikilizaji na watazamaji wajue. Manahodha wa vipindi wanafaa kuwatangazia wasikilizaji waziwazi kwamba maoni hayo hayaonyeshi kwa ukweli hisia za umma kuhusu masuala yanayojadiliwa kwenye vipindi hivyo.
c) Manahodha wanafaa kuzingatia kanuni ya haki kila wanaposoma jumbe hizo ili kuwakilisha misimamo tofauti tofauti inayotolewa na wasikilizaji
d) Wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari wanapaswa kujiepusha na mwenendo wa kufanya kura ya maoni na kuchapisha matokeo ya kura hizo kwenye kurasa zao binafsi za mitandao.

## 22. Matangazo ya moja kwa moja, simu zinazopokewa studioni na vipindi vya mijadala

Katika kushughulikia matangazo ya moja kwa moja, simu zinazopokelewa studioni na vipindi vya mijadala manahodha na watayarishaji vipindi hivyo wanafaa:

i) Kuzingatia kanuni za utendakazi wa kazi ya uanahabari kila wanapoendesha vipindi hivyo

ii) Kuzingatia ushauri wa Miongozo ya kuangazia uchaguzi na masharti mengine muhimu kuhusiana na uchaguzi

iii) Kumdadisi au hata kukomesha mazungumzo ya mpiga simu studioni ambaye amekiuka miongozo au hata sheria hasa zinazohusu Matamshi ya chuki.

iv) Wachukulie watazamaji wasikilizaji na wapiga simu studioni kwa heshima, kwa ukweli na haki.

v) Heshimu faragha na maisha binafsi ya wapiga simu studioni na vilevile kutoaingilia maisha yao binafsi.

vi) Tumia teknolojia ya kisasa inayochelewesha upeperushaji wa matangazo ili kuondoa matamshi ya kuchukiza ambayo hutokea hivi hivi tu kabla yaujumbe kupeperushwa.

vii)Toa onyo au omba radhi (mwanzo wa kipindi na mwisho wa kipindi) kwamba maoni yanayotolewa na wapiga simu kwenye kituo ni yao binafsi wala sio maoni na misimamo ya Shirika la Habari linaloongoza stesheni hiyo.

## 23. Matangazo ya kusifia wanasiasa na habari zinazolipiwa ili kupeperushwa/ kuchapishwa

Tunaposema matangazo yanayowasifia wanasiasa na habari zinazolipiwa tunamaanisha ujumbe wowote ambao wateja wa vyombo vya habari wanavipokeza vyombo vya habari wakiwa wamelipia kupeperushwa/kuchapishwa kwake. Matangazo hayo hutumika kuwaongezea sifa wanasiasa, vyama vya siasa, kuuza sera na mawazo yao kwa jamii. Katika kushughulikia matangazo kama hayo, vyombo vya habari vinapaswa:

a) Kuhakikisha usawazishaji baina ya wagombeaji kwenye namna ya kutoa muda wa kupeperusha matangazo hayo. Kumaanisha kwamba chombo kikitoa muda wa matangazo kwa mgombeaji fulani au chama fulani yafaa pia wagombeaji wengine na vyama vingine vipewe nafasi ile ili kulipia matangazo kama hayo kwenye chombo hicho.

b) Hakikisha upo usawazishaji kwenye mpango wa kuvipa vyama na wagombeaji nafasi ya bila malipo kupeperusha matangazo yanayowasifia. Kumaanisha kwamba iwapo chombo cha habari kimeamua kutoa nafasi kwa wanasiasa kupeperussha matangazo

hayo basi yafaa nafasi ile itolewe kwa wagombeaji wote na vyama vyote vilivyomo mashindanoni.

c) Hakikisha kwamba matangazo ya kuwasifia wanasiasa na habari za kulipiwa zote zimetambuliwa ifaavyo. Kwenye televisheni matangazo hayo yanafaa kuandikwa moja kwa moja kuwa ya kulipiwa kumsifia fulani- kwenye rediyo yafaa kuwe na tangazo kwenye mwanzo wa kipindi na mwisho wake.

d) Hakikisha kwamba wanahabari na washirika kwenye vyombo vya habari hawahusiki kwenye matangazo ya kuwasifia wanasiasa mfano kwa kuvaa mavazi yenye rangi na nembo za vyama vya kisiasa.

e) Kagua matangazo ya kusifia vyama vya siasa na wanasiasa na habari zinazolipiwa kuelewa yaliyomo kwenye matangazo hayo; Tathmini ubora wake, iwapo yanashirikisha matamshi yasiyofaa, yana haki, ukweli, yanaweza kupalilia majibizano, yatamharibia yeyote sifa, au yanajumuisha picha na michoro ya kuchukiza. Matangazo ya kusifia vyama vya siasa na wanasiasa yanafaa kuwa na majina haswa ya wafadhili, na pale inapofaa, nembo zao na kwamba yasichapishwe bila kujulikana asili yake.

Vyombo vya utangazaji vilevile vinapaswa kutii maelekezo ya Kanuni za Uandaaji Vipindi kwa ajili ya Rediyo na televisheni ambazo masafa yake hutolewa bila malipo Mwaka 2016 zilizochapishwa na Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya. Kanuni hiyo inasema kwamba Rediyo na Televisheni zina wajibu wa kuuhudumia umma.

Maadili yanayoongoza matangazo ya kusifia hutaka kwamba:

i) Haki ya raia na makundi kujitetea iwapo yameshambuliwa kwenye vipindi vilivyopeperushwa inalindwa (nafasi ya kujieleza ipo)

ii) Matangazo ya kusifia yanatenganishwa na taarifa za habari na vipindi vya habari

iii) Upo usawazishaji kwenye mpango wa wagombeaji kupata matangazo ya kusifia, ikiwemo gharama za malipo na muda wa kupeperushwa.

iv) Habari zinazopeperushwa kimaandishi kwenye televisheni haziwezi kutumiwa kama matangazo ya kusifia wakati wa taarifa za habari

v) Matangazo ya kusifia hayatakiuka kanuni ya kuwaheshimu watu.

vi) Matangazo ya kusifia yanayokiuka desturi, imani za kidini na imani za kisiasa hayataruhusiwa

vii) Matangazo ya kusifia hayatapeperushwa kwa muda za zaidi ya dakika kumi kwenye kipindi cha televisheni cha dakika 30 au zaidi ya thuluthi moja ya muda wa kipindi.

## UTEKELEZAJI MIONGOZO HII

### 24. Miongozo ya uhariri /sera za vituo vya habari

Ili kutekeleza miongozo hii kwa ufanisi, taasisi za vyombo vya habari zinapaswa:

a) Kutumia miongozo hii kwa kuishirikisha na sera zao za vyumba vya habari na kanuni za uhariri za ndani.

b) Kuchapisha miongozo hii kwa pamoja na Kanuni za ndani na sera za vyumba vya habari kuhakikisha upo uelewa wa kutosha ili kuuwezesha umma kufuatilia namna ambavyo vyombo vya habari vinazingatia kanuni hizo kazini.

c) Hakikisha shughuli ya kuangazia uchaguzi imepangwa vyema na raslimali za kufanikisha hayo zimetengwa.

d) Jenga mfumo wa kufuatilia au kuhakiki namna ambavyo Kanuni ya utandakazi zinazingatiwa.

### 25. Malalamiko

Katika msimu wa uchaguzi, malalamiko yanafaa kushughulikiwa na kusuluhishwa kwa haraka tena kwa njia ya haki. Mbali na njia za ndani ya vyumba vya habari za kusuluhisha malalamiko, wakiwemo wahariri-umma, Kamati ya Baraza la Vyombo vya habari inayoshughulikia Malalamiko inafaa kutoa umuhimu wa kwanza kwa malalamiko ya msimu wa uchaguzi-hasa yanayotolewa na umma. Suluhisho kwa malalamiko haya zafaa kupewa vyombo vya habari mara moja, ikiwamo washika dau katika sekta ya vyombo vya habari. Vyombo vya habari vinafaa kutangaza matokea ya usuluhishaji wa malalamiko yanayowahusu.

### Malalamiko hutolewa vipi?

Yeyote anayehisi kudhulumiwa na chombo cha habari anaweza kutoa malalamiko, iwe kwa matamshi tu, awe ameelekea katika afisi za Baraza au kwa kutuma waraka, iwe kwa njia ya elektroniki, au aandike barua imfikie msajili wa Kamati ya Malalamiko akielezea msingi wa malalamiko yake, namna ambavyo amedhulumiwa, huku akielezea namna anafaakufidiwa.

### 26. Kufuatilia kazi ya Vyombo vya habari

Vyombo vya habari vinafaa kuwa na njia na mifumo ya kufuatilia namna ambayo vinaangazia uchaguzi. Vyombo vinafaa kujenga sera zinazosimamia uhifadhi wa matangazo na vipindi vyake ikiwemo habari zilizoperushwa kwenye mitandao. Televisheni na Rediyo zafaa kuhifadhi kwa zaidi ya siku 90 (tangu siku ya kupeperushwa) nakala za matangazo yote yaliyopeperushwa msimu wa uchaguzi. Wachapishaji wa habari mitandaoni na vyombo vya dijitali wanafaa kuhifadhi rekodi za taarifa zao kwa siku 60 tangu ufanyike uchaguzi.

Baraza la Vyombo vya habari litafuatilia utendakazi wa vyombo vya habari kuhusiana na

namna vinazingatia kanuni za utendakazi na uzingatiaji wa kutoka nafasi sawa kwa vyama vya siasa na wagombeaji. Baraza litatoa taarifa kila mwezi kuhusu ufuatiliaji huu – taarifa hizo zitahusu namna vyombo vya habari vimeangazi uchaguzi. Vyombo vya habari vinafaa viwe tayari kurekebisha mielekeo hasi kwenye utendaji wake baada ya ukaguzi na tathmini zinazotangazwa kwenye ufuatiliaji na uhakiki.

## MAREJEO/DONDOO

*AGENDA: Media Guidelines for Reporting on Accessible Elections; Indonesian Edition, 2015*

*ARTICLE 19 – "Hate Speech" explained: a toolkit, 2015*

*ARTICLE 19: Guidelines for Election Broadcasting in Transitional Democracies*

*Association of Caribbean Media Workers: An Election Handbook for Caribbean Media Workers*

*BBC Election Guidelines, 2015*

*Centre for International Media Assistance: Covering elections - The challenges of training the watchdogs*

*Constitution of Kenya: Laws of Kenya 2010*

*Ethical Journalism Network – A Checklist for hate speech*

*GJA (Ghana Journalists Association) Guidelines on Election Coverage*

*Guidelines and Principles for Broadcast Coverage of Elections in the SADC Region*

*Guidelines for Reporting Elections in Liberia*

*INTERMEDIA: Reporting for change: a handbook for journalists covering elections (in Pakistan), 2008*

*Media Council of Kenya: Code of Conduct and Practice of Journalism in Kenya, 2013*

*Media Council of Kenya: Guidelines for Election Coverage in Kenya, 2017*

*Public Policy Institute (PPI) - Guidelines for Gender Sensitive Reporting*

*Reporters without Borders and the International Organization of La Francophonie (OIF) –*

*Handbook for Journalists during Elections*

*SANEF: Helpful Guidelines for Journalists Covering the Election*

*The Nigerian Media Code of Election Coverage, 2014*

*UNDP media-and-elections-guide-electoral-practitioners*

*UNDP - UNDP Gender Responsive National Communications Toolkit, 2015*

*UNESCO/Ross Howard: Conflict Sensitive Reporting: State of the Art, 2009*

## KIAMBATISHO CHA 1

## MKATABA WA MAAZIMIO 12 YA WAMILIKI VYOMBO VYA HABARI, MAMENEJA NA WAHARIRI KUWAHAKIKISHIA WANAHABARI USALAMA

Serikali, Vyombo vya habari, wamiliki Vyombo, mameneja na wahariri ndilo kundi la mbele lenye wajibu mkubwa wa kuhakikisha upo uhuru wa kujieleza na kutoa habari huku mwanahabari akihakikishiwa usalama wake. Kwa hivyo ni jukumu lao la kikazi kuhakikisha kwamba wametoa mazingira salama kufanyika uanahabari. Hali hiyo ndiyo lengo haswa lililotangazwa kwenye Mpango wa Matendo wa Umoja wa Mataifa kuhusu Usalama wa Wanahabari kukomesha mwenendo kudhulumu bila hofu ya kuchukuliwa hatua. Kutokana na haya, wasimamizi wanafaa kuanzisha matawi ya usalama kwenye vyumba vya habari ili kutekeleza, kufuatilia na kuhakikisha masharti yafuatayo yamezingatiwa:

1) Angalia kwa umakini ili kuelewa swala la tishio kwa wanahabari halafu hakikisha kwamba mwanahabari anaelewa kwa ukamilifu. Vilevile mpe miongozo ya namna ya kuripoti matukio yanayotishia usalama wake bila kumlazimisha ili aamue mwenyewe kuyazingatia au akatae
2) Wanahabari wanaofuatilia matukio ambayo ni hatari kwa usalama wanafaa kupewa mafunzo kuhusu namna ya kukabili mambo yanayohatarisha usalama wao; masomo hayo hufunza huduma ya kwanza, sheria za kimsingi za kufuata na usaidizi wa kisaikolojia.
3) Toa mafunzo na ushauri wa mara kwa mara unaoambatana na namna ya matukio ambayo mwanahabari anayafuatilia
4) Waorodheshe wanahabari kwenye huduma za bima ya kuwalinda kutokana na kujeruhiwa wakiwa kazini, tishio la kupoteza maisha, mali na vifaa vya kazi.
5) Toa usaidizi wa kisheria kupitia kutetewa na mawakili ikiwa njia ya kukabili mwenendo wa watu kufanya makosa bila hofu ya kuadhibiwa.
6) Toa ufadhili wa raslimali ya kuwezesha kazi kufanyika; huduma za uchukuzi, mavazi ya kuvaliwa wakati wa kufuatilia matukio yanayotishia maisha na pesa kwa wanahabari wanaofuatilia matukio ya kutisha.
7) Toa huduma za mara kwa mara za kuboresha maisha yao ikiwemo kuwapa ushauri nasaha, hasa baada ya kazi ya kufuatilia matukio ya kutatiza na yanayopalilia majonzi.
8) Jenga mpango kamilifu wa kusimamia maswala ya usalama, ikiwemo njia za kuingilia ili kuwasaidia wanahabari kukitokea hatari mfano kuwaondoa mahala penye hatari na shirika liwe na meneja wa usalama anayewafadhili wanahabari.

9) Anzisha hazina ya fedha ya kuwafadhili wanahabari huru wanaohudumia shirika, ambao wanafuatilia kazi ya unanahabari waliyopewa na chumba cha habari. Hazina hiyo inafaa iwe mfuko wa michango ya kila mwaka ya mashirika ya habari au mapato ya Baraza la Vyombo vya habari yanayokusanywa kupitia faini ambazo baraza linatoza vyumba vya habari na wanahabari wanaohusika makosa.

10) Anzisha taratibu mahsusi za kuwalinda wanahabari wanaoathirika kwa matukio yanayoegemea jinsia mfano dhuluma za kimapenzi.

11) Anzisha madawati ya kufuatilia na kufichua uongo na yale ya utafiti ikiwa njia ya ku kurekebisha pakitokea habari za uongo kuenea na vilevile kuchapisha taarifa zisizo za ukweli ambazo hupalilia ukosoaji mkali dhidi ya wanahabari wa shirika.

12) Masharti ya kuzuia ueneaji wa janga la Korona (Covid-19) yalijumuisha taratibu zote za kumlinda mtu iwe yupo ndani ya chumba cha habari au yupo nje

## RATIBA YA UCHAGUZI MKUU - 2022

### a. Uteuzi kwenye vyama vya siasa

| No. | Shughuli | Kuanza | Kumaliza | Muda |
|---|---|---|---|---|
| **1** | **UTEUZI KWENYE VYAMA** | **Oktoba 18, 2021** | **Juni 24, 2022** | |
| **1.1** | Kukamilika kwa michango ya wagombeaji | Desemba 09, 2021 | Desemba 09, 2021 | Miezi 8 kabla ya kufanyika uchaguzi |
| **1.2** | Kujiuzulu kwa maafisa wa serikali wanaonuia kugombea viti uchaguzini | Februari 09, 2022 | Februari 09, 2022 | Miezi 6 kabla ya uchaguzi |
| **1.3** | Kuwasilisha sheria za vyama za kuongoza shughuli ya uteuzi vyamani mbele ya IEBC | | Oktoba 18, 2021 | Miezi 6 kabla shughuli ya uteuzi |
| **1.4** | Kuwasilisha marekebisho yoyote kwenye sheria za uteuzi | Oktoba 18, 2021 | Januari 16, 2022 | Siku 90 baada ya kuwasilisha sheria |
| **1.5** | Vyama kuwasilisha mbele ya IEBC sajili ya wanachama | | Aprili 09, 2022 | Siku 120 kabla ya uchaguzi |
| **1.6** | Kuwasilisha mbele ya IEBC majina ya wagombeaji wa nyadhifa kwenye uteuzi | | Aprili 09, 2022 | Siku 21 kabla kufanyika uteuzi |
| **1.7** | Kuwarasimisha wagombeaji na tarehe ya kufanyika shughuli ya uteuzi | Aprili 09, 2022 | Aprili 16, 2022 | Siku 7 baada ya kupokea majina |
| **1.8** | Vyama vinahusika uteuzi | Aprili 16, 2022 | Aprili 22, 2022 | |
| **1.9** | Shughuli ya kusuluhisha mizozo chini ya Taasisi ya tume ya kushughulikia mizozo | Aprili 25, 2022 | Mei 06, 2022 | |

## RATIBA YA UCHAGUZI MKUU - 2022

### b. Uteuzi kwenye vyama vya siasa

| No. | Shughuli | Kuanza | Kumaliza | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1.11 | Wanasiasa wenye nia ya kugombea-huru wasiwe wanachama wa chama chochote | | Mei 09, 2022 | Siku 90 kabla uchaguzi mkuu |
| 1.12 | Wagombea-huru kuwasilisha mbele ya IEBC nembo zao, barua ya kuomba kushiriki, na barua ya idhini ya Msajili wa vyama | | Mei 02, 2022 | Siku 21 kabla kuteuliwa na Tume |
| 1.13 | Idhini ya IEBC ya nembo za vyama na wagombea-huru | Mei 09, 2022 | Mei 09, 2022 | |
| 1.14 | Kurasimisha majina na nembo za wagombea-huru | Mei 09, 2022 | Mei 13, 2022 | Siku 14 kabla ya kuteuliwa na Tume |
| 1.15 | Kuwasilisha nembo za vyama vya siasa, majina na nakala ya saini za wawakilishi wa vyama, ili kuidhinisha uteuzi kwenye vyama mbali mbali na wale wameteuliwa | Januari 16, 2022 | Mei 06, 2022 | |
| 1.16 | IEBC inawapa wasimamizi wa uchaguzi nyanjani nakala za walioidhinishwa kusaini mambo ya vyama na nembo za wagombeaji | Mei 09, 2022 | Mei 16, 2022 | |
| 1.17 | Mkutano wa kabla uteuzi baina ya IEBC na wagombeaji | Mei 16, 2022 | Mei 22, 2022 | |
| 1.18 | Kuchukua stakabadhi za uteuzi na Kanuni za Utendakazi | Mei 09, 2022 | Juni 10, 2022 | |
| 1.19 | Uwasilishaji na ukaguzi wa orodha ya wagombeaji urais | Mei 23, 2022 | Mei 25, 2022 | Siku 5 kabla uteuzi wa wanaogombea urais |

## RATIBA YA UCHAGUZI MKUU - 2022

### a. Uteuzi kwenye vyama vya siasa

| No. | Shughuli | Kuanza | Kumalizika | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1.20 | Kuteuliwa kwa ajili ya kugombea urais | Mei 30, 2022 | Juni 10, 2022 | Siku 60 kabla uchaguzi mkuu |
| 1.21 | Kuteuliwa kwa ajili ya kugombea useneta | Mei 30, 2022 | Juni 02, 2022 | Siku 60 kabla uchaguzi mkuu |
| 1.22 | Kuteuliwa kwa ajili ya kugombea ubunge | Mei 30, 2022 | Juni 01, 2022 | Siku 60 kabla uchaguzi mkuu |
| 1.23 | Kuteuliwa kwa ajili ya kugombea wadhifa wa mwakilishi wadi | Juni 02, 2022 | Juni 10, 2022 | Siku 60 kabla uchaguzi mkuu |
| 1.24 | Kuteuliwa kwa ajili ya kugombea wadhifa wa mwakilishi wa kike | Juni 03, 2022 | Juni 06, 2022 | Siku 60 kabla uchaguzi mkuu |
| 1.25 | Kuteuliwa kwa ajili ya kugombea Ugavana | Juni 07, 2022 | Juni 10, 2022 | Siku 60 kabla uchaguzi mkuu |
| 1.26 | Kuwasilisha malalamiko yanayotokana na shughuli ya uteuzi na usuluhishi wake | Juni 10, 2022 | Juni 20, 2022 | Siku 10 baada ya kuwasilisha malalamiko |
| 1.27 | Uchapishaji wa majina ya wanasiasa wote walioteuliwa | Juni 20, 2022 | Juni 24, 2022 | |
| 1.28 | Vyama kuwasilisha mbele ya IEBC orodha za majina ya wagombeaji | | Juni 25, 2022 | Siku 45 kabla uchaguzi |

## SHUGHULI ZA KABLA UCHAGUZI

| No. | Shughuli | Kuanza | Kumalizika | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 3.0 | SHUGHULI ZA KABLA UCHAGUZI | Jumatatu, Machi 07, 2022 | Jumanne, Agosti 09, 2022 | |
| 3.1 | Ilani ya kufanyika uchaguzi mkuu | | Machi 14, 2022 | |
| 3.2 | Uteuzi wa maafisa wasimamizi wa uchaguzi na manaibu wasimamizi | | Machi 14, 2022 | |
| 3.3 | Kusambaza orodha ya majina ya maafisa wasimamizi kwa vyama vya siasa | Machi 14, 2022 | Machi 28, 2022 | |
| 3.4 | Maagizo ya kabla uchaguzi kwa wasimamizi - uchaguzi kitaifa | Machi 28, 2022 | Aprili 03, 2022 | |
| 3.5 | Maafisa wasimamizi-uchaguzi wasaini Kanuni za utendakazi | Machi 28, 2022 | Aprili 03,2022 | Katika mkutano wa kupanga uchaguzi |
| 3.6 | Kuhakiki vituo vya kupigia kura na vituo vya ujumuishaji kura katika daraja tofauti tofauti | Mei 02, 2022 | Mei 22, 2022 | |
| 3.7 | Kurasimisha vituo vya kupigia kura na vituo vya ujumuishaji | Juni 20, 2022 | Juni 24, 2022 | |
| 3.8 | Uteuzi wa maajenti-uchaguzi katika maeneo bunge na kaunti | | Julai 10, 2022 | Siku 21 kabla ya uchaguzi |
| 3.9 | Uteuzi wa maajenti wakuu | Julai 19, 2022 | Julai 10, 2022 | |
| 3.10 | Usajili wa maafisa wa uchaguzi (wasimamizi wa vituo, manaibu wao, na makarani) | Machi 28, 2022 | Mei 27, 2022 | |
| 3.11 | IEBC kuvisambazia vyama orodha ya majina ya wagombeaji walioteuliwa. | Mei 27, 2022 | Juni 10, 2022 | |


## SHUGHULI ZA KABLA UCHAGUZI

| No. | Shughuli | Kuanza | Kumaliza | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 3 | SHUGHULI ZA KABLA UCHAGUZI | Jumatatu, Machi 07, 2022 | Jumanne, Agosti 09, 2022 | |
| 3.12 | Kupitia kauli za vyama vya siasa na washikadau | Juni 10, 2022 | Juni 24, 2022 | |
| 3.13 | Kuchapisha orodha ya mwisho ya wagombeaji na kuwapa maafisa wanaosimamia uchaguzi vituoni | Juni 27, 2022 | Agosti 01, 2022 | |
| 3.14 | Mafunzo kwa maafisa wa uchaguzi na maandalizi mengine | Julai 01, 2022 | Agosti 06, 2022 | |
| 3.15 | Mafunzo na kuapishwa kwa maafisa wa usalama | Agosti 01, 2022 | Agosti 05, 2022 | |
| 3.16 | Ukaguzi wa vituo vya kupigia kura na mjarabu wa njia za kupeperusha matokeo | Agosti 01, 2022 | Agosti 05, 2022 | |
| 3.17 | Kutundika sajili ya wapiga kura katika vituo vya kupigia kura | | Agosti 01, 2022 | Siku 7 kabla ya siku ya uchaguzi |
| 3.18 | Kuwatuma maafisa-huduma wa vituo vya kura na vifaa vya uchaguzi | Agosti 08, 2022 | Agosti 08, 2022 | |

## SIKU YA UCHAGUZI, KUSIMAMIA UTOAJI MATOKEO

| No. | Shughuli | Kuanza | Kumaliza | Muda |
|---|---|---|---|---|
| **4** | **SIKU YA UCHAGUZI, KUSIMAMIA MATOKEO** | **Agosti 09, 2022** | **Agosti 28,2022** | |
| 4.1 | Vituo vya kura kufunguliwa saa kumi na mbili asubuhi, kufungwa saa kumi na moja jioni | Agosti 09, 2022 | Agosti 09, 2022 | |
| 4.2 | Hesabu ya kura, ujumuishaji wa kura kwenye vituo | Agosti 09, 2022 | Agosti 10, 2022 | |
| 4.3 | Kupeperusha(kielektroniki) matokeo kutoka vituoni | Agosti 09, 2022 | Agosti 10, 2022 | |
| 4.4 | Ukusanyaji matokeo ya urais katika maeneo bunge na kuyatangaza | Agosti 09, 2022 | Agosti 12, 2022 | |
| 4.5 | Ujumuishaji, kuthibitisha na kutangaza matokeo ya urais katika kituo kikuu cha ujumuishaji cha taifa | Agosti 09, 2022 | Agosti 15, 2022 | |
| 4.6 | Ukusanyaji na kutangaza matokeo yote | | Agosti 15, 2022 | |
| 4.7 | Kurasimisha matokeo ya Uchaguzi, kupitia gazeti rasmi la serikali | Agosti 15, 2022 | Agosti 28, 2022 | |
| 4.8 | Kuandaa nakala na kuchapisha fomu za matokeo | Agosti 09, 2022 | Agosti 28, 2022 | |

## MDUARA WA UCHAGUZI



MEDIA
COUNCIL OF KENYA

BARAZA LA VYOMBO VYA HABARI

Mawasiliano Muhimu

Orofa ya chini,
Jengo la Britam Centre,
Mara /Ragati Road Junction, Upper hill,
S.L. Posta 43132 -00100 Nairobi, Kenya
Nambari ya Simu: +254(020)2737 58/+254(020) 271 6266,
Simu ya Rununu: +254(0) 727 735 252
Barua Pepe: info@mediacouncil.or.ke
www.mediacouncil.or.ke